# FORM 2 TERM 3 2020
# KISWAHILI

**1. <u>UFAHAMU</u> (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo uliwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malighafi inayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu sana kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda . Katika msingi huu viwanda vikubwa vitawiwa ugumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vinao uwezo wa kuwaajiri wafanyikazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyikazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la ajira ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasmia (yenye viwanda vingi) mataifa mengi yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujarisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapanu, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hiyo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa yenyewe. Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo.

Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimezambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huo wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

a) Kwa nini viwanda ni muhimu? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

b) Ni nini kiini cha matatizo ya uuzaji wa bidhaa katika nchi zinazoendelea? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………..

c) Eleza faida zinazotokana na kuwepo kwa viwanda vidogo vidogo. (alama 4)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………..

d) Usambazaji wa viwanda katika maeneo ya mashambani una faida gani? (alama 4)

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………..

e) Fafanua maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 3)

i. Kujasurisha

……………………………………………………………………………………………………….

ii. Amali

……………………………………………………………………………………………………….

iii. Utashi

……………………………………………………………………………………………………….

2. **UFUPISHO (ALAMA 15)**
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayaofuata.**

Tume ya kutathmini mishahara (SRC) inafaa kuchunguza kwa makini pendekezo la kutaka umri wa kustaafu kwa watumishi wa uma upunguzwe kutoka miaka 60 hadi 55.

Kulingana na SRC, kupunguzwa kwa umri wa kustaafu kutasaidia kupunguza mzigo mzito wa mishahara ambayo hupewa wafanyikazi wa umma na kuacha kiasi kidogo tu cha fedha wa ajili ya miradi ya maendeleo. Kufanya hivyo ni sawa na kukata mguu kwa sababu una kidonda kabla ya kuutafutia matibabu.

Ikumbukwe kuwa, umri wa kustaafu kwa watumishi wa umma nchini uliongezwa miaka mitano iliyopita kutoka miaka 55 hadi 60 baada ya Serikali kung'amua kuwa zaidi ya wafanyikazi 20,000 wa umma na walimu walitaka kulipwa pensheni, hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali.

Wakati mjadala wa kutaka kupunguza mishahara minono ambayo watumishi wa umma wanapokea na kuacha masazo kwa ajili ya maendeleo kuzuka mwezi Machi, mwaka hu, Rais, naibu wake pamoja na baraza la mawaziri walitangaza mishahara yao ipunguzwe. Rais pia aliwashinikiza wakuu wa mashirika ya umma kufuata nyayo la sivyo wapigwe kalamu nyekundu.

Mathalani, wasomi wa masuala ya uchumi nchini China, ambapo umri wa wastani wa kustaafu ni miaka 53, wanajikuna kichwa sasa ili kutafuta mikakati ya kuongeza umri huo hadi miaka 65 katika kipindi cha miongo miwili ijayo kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kinachotumika kuwalipa wanaostaafu pensheni zao.

Wasomi wa uchumi nchini humo wanadai kuwa pengo lililopo, baina ya umri wa kustaafu wa miaka ma wastani wa umri ambao. Wachina wanastahili kuishi wa miaka 75, ni kubwa mno hivyo kuongeza uwezekano wa mtu kuendelea kuchukua malipo ya baada ya kustaafu kwa zaidi ya miaka 10. Kwa mujibu

wa wanauchumi, hali hiyo imesababisha Msongamano mkubwa katika hazina ya malipo ya uzeeni. Suala hilo lilisababisha Serikali kualika masharika mbalimbali duniani yakiwemo Benki ya Dunia na Shirika la Wafanyikazi Ulimwenguni (ILO) kutoa mapendekezo ya kuhusiana na hali hiyo.

Benki ya Dunia ilishauri China kuongeza umri wa kustaafu ili kupunguza kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika kulipa waliostaafuu malipo ya baada ya uzeeni. Nchini Uturuki, mtu anatakiwa kustaafu baada ya kuifanya kazi kwa kipindi cha miaka 25. Hiyo inamaanisha kuwa mtu akianza kuifanya kazi akiwa na umri wa miaka 20 atatakiwa kustaafu anapotimiza miaka 45.

Hata hivyo, hatua hii ya kustaafisha watu mapema, imekuwa na athari chungu nzima kiuchumi nchini humo huku ikikadiriwa kuwa kufikia mwaka wa 2045 taifa hilo litakuwa likitumia asilimia 6 ya mapato yake kulipa pensheni, endapo mambo hayatabadilishwa.

Hayo ni mataifa machache kati ya mengi ambayo yamejaribu kupunguza umri wa kustaafu na kujutia baadaye. Serikali inafaa kutafuta njia mbadala kukabiliana na tatizo hilo na wala sio kuwaachisha kazi mapema.

(a) Kwa maneno yasiyozidi 50, Eleza sababu za kuoengeza umri wa kustaafu kutoka miaka 55 hadi 60 na athari zake. (Alama 7)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………….

(b) Kwa maneno yako mwenyewe Fupisha aya tatu za mwisho. Tumia maneno 70. (Alama 8)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………….

NAKALA SAFI

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….

**3. MATUMIZI YA LUGHA.** **(ALAMA 40)**

(a) Taja sifa tatu kuu za sauti /k/. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….

(b) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (alama 5)

i. Uhusiano wa baba huyu una mvuto mkubwa

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

ii. Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………......

(c) Andika kinyume cha;

Wazee walifukua shimo lililpfunikwa. (Alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………….

(d) Andika kwa wakati ujao: Ungalifanya kazi kwa uaminifu usingalipigwa kalamu. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(e) Unda vitenzi kutokana na vivumishi vifuatavyo. (alama 2)

(i) Bora

…………………………………………………………………………………………………………

(ii) Refu

…………………………………………………………………………………………………………

(f) Tunga sentensi nne kuonyesha matumizi tofauti ya alama ya kinukuu. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(g) Kanusha sentensi zifuatazo. (alama 4)

i. Watoto wametembea.

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………….

ii. Watatunza Jona na Hamisi.

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………….

(h) Nomino zifuatazo ni za ngeli zipi ? (alama 4)

I. Shimoni

…………………………………….

II. Sukari

…………………………………….

III. Uji

……………………………………

IV. Mijusi

…………………………………….

(i) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali zilizomo mabanoni. (alama 4)

I. Tembea (tendesha)

……………………………………………………………………………………………………..

II. *Ku*la (tendewa)

……………………………………………………………………………………………………..

III. Lima (tendeshana)

……………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………..

(j) Andika katika ukubwa. (alama 4)

I. Chungu kilichovunjika kilikuwa kipya.

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

II. Mto huo umefurika.

…………………………………………………………………………………………………………..

(k) Unda nomino moja moja kutokana na : (alama 3)

I. Kulea

………………………………………………..

II. Fikiria

………………………………………………..

III. –erevu

………………………………………………..

(l) Bainisha vielezi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Mlevi aliyelewa chakari ataelekea nyumbani jioni.

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

4. **ISIMU JAMII(ALAMA 10)**

| | |
|---|---|
| Jera: | Mbili kwa hamsini! Moja kwa thirty! Leo ni bei ya hasara! |
| Reja: | Unauza hii tight kwa pesa ngapi? |
| Jera: | Hiyo ni eighty bob mtu wangu |
| Reja: | Huwezi kunipunguzia. Niuzie forty hivi. |
| Jera: | Haiwezekani mtu wangu. Nitapata hasara nikiuza hivyo. Ongeza mbao, brother. |
| Reja: | Basi hamsini na tano. |
| Jera: | Tafadhali ongeza kitu kidogo. Unataka nikule hasara leo? Fikisha sitini. |
| Reja: | Sawa basi nitanunua. Shika sixty bob. |
| Jera: | Asante Customer. Mungu akubariki. |

(a) Tambua sajili hii. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

(b) Huku ukitoa mifano, eleza sifa nne za sajili hii. (alama 8)

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………